

# Sauti za Vijana

## Maoni ya vijana kuhusu elimu jumuishi

the atlas alliance
global support to disabled people

# Sauti za Vijana

## Maoni ya vijana kuhusu elimu jumuishi

OPERASJON DAGSVERK

nfu
Norsk Forbund for Utviklingshemmede

NAD
equal rights and full participation

the atlas alliance
global support to disabled people

**Kimechapishwa na:**

The Atlas Alliance
Schweigaardsgt 12
S.L.P. 9218 Gronland
Simu: +47 22 17 46 47
Faksi: +47 23 16 35 95
Barua pepe: atlas@atlas-alliansen.no
Tovuti: www.atlas-alliansen.no

**Chapa ya kwanza:** Septemba 2008

Hiki kitabu kimetayarishwa na Ingrid Lewis. Filamu (DVD) inayoambatana
na kitabu hiki imetayarishwa na kuhaririwa na Åse Drivenes. Kimetafsiriwa na Evena Massae.

Kitabu hiki pia kinapatikana kwenye tovuti za Atlas Alliance
(www.atlas-alliansen.no) na Enabling Education Network
(www.eenet.org.uk)

Nakala za filamu (DVD) zinapatikana kutoka EENET, c/o ESI, School of Education,
University of Manchester, Oxford Road, Manchester, M13 9PL, UK
Barua pepe: info@eenet.org.uk.

Picha ya jalada na Ingrid Lewis

# Yaliyomo


Shukrani ........................................................ 2

Utangulizi ........................................................ 3

Maoni ya wanafunzi kuhusu elimu jumuishi .......... 11

Mazingira ........................................................ 11

Sera ........................................................ 22

Matendo ........................................................ 24

Raslimali ........................................................ 33

Mitazamo ........................................................ 40

Baadhi ya maoni ya mwisho ................................ 46

# Shukrani

Kitabu hiki kisingewezekana kutayarishwa kama siyo uchangamfu, kujitoa na hekima waliyoonyesha wanafunzi walioshiriki katika mradi wa **Sauti za Vijana**. Hatuwezi kuwashukuru vya kutosha kwa jinsi walivyoshirikiana nasi na dunia nzima kuhusu undani wao na wanavyojisikia kuhusu elimu yao. Tunategemea kuwa wataendelea kuongea na kutoa ushauri jinsi ya kuboresha elimu ili iwe jumuishi kwa kila mmoja. Shukrani zetu pia ziwaendee wazazi wa Ally Iddi na walezi wa Omari Chota kwa ukarimu waliyoonyesha tulipowatembelea nyumbani kwao.

Tungependa kuwashukuru wafanyakazi kutoka Shule ya Msingi Agururu na Shule ya Sekondari ya Rock huko Tororo, nchini Uganda na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa kilichopo Morogoro, nchini Tanzania kwa kufanikisha mradi huu na kuwaruhusu wanafunzi wao kushiriki.
Nchini Tanzania tunapenda kushukuru Chama kwa Ajili ya Wenye Ulemavu wa Akili Tanzania (TAMH), Evena Massae, Pulcheria Ndamgoba, Abdallah Mng`obwa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Huko Uganda shukrani zetu ziwaendee Moses Moiza, Simon Obbo, Wizara ya Jinsia, Kazi na Huduma za Jamii, pamoja na Idara ya Ulemavu na Wazee, uongozi wa wilaya ya Tororo na watumishi wa Idara ya Elimu.

Mwisho, shukrani zetu ziwaendee mashirika ya Atlas Alliance na Operation Days Work kwa kufadhili mradi wa **Sauti za Vijana**.

**Ingrid Lewis, project facilitator**
**Åse Drivenes, film-maker**

# Utangulizi

## Elimu Jumuishi

Duniani kote, vijana wengi hawana uwezo wa kwenda shule kwa sababu ya umaskini na kutengwa. Wanaweza kutengwa kwa mfano kwa sababu ni walemavu, wasichana, wakimbizi, vijana wanaofanya kazi au kutoka kwenye kikundi cha jamii, dini au lugha fulani. Hata kwa wale vijana wanaobahatika kwenda shule wengi wanajitahidi kujihusisha katika masomo lakini humaliza bila kujifunza mambo ya kutosha.

Elimu jumuishi inajumuisha mabadiliko yavitu vitu vingi sana shuleni au mfumo mzima wa elimu wa nchi, ili vijana wote wajisikie kukaribishwa, kuingia shuleni na kuweza kufaidika na elimu itolewayo hata kama siku za nyuma waliachwa.

Watu wengi wanafikiri elimu jumuishi ni kufanya tu shule ziwe na mazingira yanayofikika na wanafunzi wenye ulemavu. Lakini elimu jumuishi ni mambo magumu zaidi.Inahitaji kujua nyanja zote na uzoefu wa vijana kupata elimu na kujua na kufanya mabadiliko madogo na makubwa yatakayochukuwa muda mrefu. Mabadiliko haya yalenge kuwawezesha vijana wengi zaidi kuhudhuria shuleni, kujumuika katika kujifunza na kwenye shughuli za kijamii na kufanikiwa kwa kiwango cha juu cha uwezo wao.

Kwa elimu kuwa jumuishi zaidi, ni lazima kuwe na mabadiliko ya mitazamo ya watu, matendo, mazingira, sera za kijamii, kitaifa na kimataifa na jinsi rasilimali zinavyogawanywa na kutumika.

# Mradi wa Sauti za Vijana

## Kwa nini tulifanya mradi huu?

Kuanzia mwaka 2003 shirika la Atlas Alliance kupitia Norwegian Association of Disabled (NAD) na Norwegian Association for Persons with Developmental Disabilities (NFU) limekuwa likisaidia miradi ya elimu jumuishi katika nchi za Malawi, Uganda, Tanzania Bara na Zanzibar. Miradi hii imeshafanyiwa tathimini na watu, wazima lakini maoni ya vijana waliohusishwa hayajawahi kuandikwa kwa usahihi. Kwa hiyo mradi wa **Sauti za Vijana** uliwataka vijana wenye ulemavu na wasio na ulemavu kueleza uzoefu wao katika elimu jumuishi. Ni nini kinachowafanya wajisikie wamejumuishwa au kutokujumuishwa kwenye elimu?

Kusudi kubwa la Mradi wa **Sauti za Vijana** ilikuwa kutayarisha kitabu na filamu, vikielezea maoni yao pamoja na kuonyesha picha zao. Lakini tunategemea kwamba itawasaidia watu wazima na vijana kufikiria kinachofanya shule zao kuwa jumuishi, kutekeleza miradi mingine ya aina hii na kufanya kazi kwa pamoja katika kutatua matatizo yatakayojitokeza ili kuhakikisha kwamba shule zinakuwa jumuishi zaidi kwa kila mmoja.

# Shughuli gani zilifanyika katika mradi huu?

Siyo kila mwanafunzi anapenda kuandika au kuongea mbele ya kikundi kikubwa cha watu au kusailiwa na watu wazima. Kwa hiyo, Mradi wa **Sauti za Vijana** ulitumia njia mbali mbali, ili kumwezesha kila mwanafunzi achague njia ya mawasiliano ambayo itamwezesha kujisikia vizuri.

## Kupiga Picha

Tuliwaonyesha wanafunzi picha zilizopigwa na wenzao kutoka shule na jamii nyingine huko Afrika na Asia. Walizijadili picha hizo na kuamua ni zipi walizozipenda au kutokuzipenda, zipi zilizoonyesha furaha au kukosa furaha na ni zipi zilizofanana au kutofautiana na uzoefu wao katika elimu, shule na jumuiya zao. Kwa kutumia picha na kuanza majadiliano kama hayo inaitwa "picha elekezi". Baadaye tuliwafundisha wanafunzi jinsi ya kutumia kamera rahisi za digitali.

Walipiga picha za mahali walipopapenda, walipopachukia, au walipopapaona panafurahisha na pasipofurahisha katika mazingira ya shule zao. Tulitumia mashine kuzisafisha picha hizo. Baadaye, wanafunzi walitengeneza mabango ya kuwek a picha zao. Baadhi ya wanafunzi waliandika maneno, walichora michoro, au waligundisha maua kwenye mabango yao ili kuzifanya picha kuwa na mng'aro na kuvutia (angalia ukurasa wa 9 kwa mfano).

Tuliwaambia wanafunzi watueleze kuhusu picha zao – wakati mwingine mmoja mmoja au kikundi kidogo au kwa kuelezea mabango yao kwa wanafunzi wote darasani.



Ally na Aron wakifanya zoezi la kutumia kamera, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa

## Kuchora

Tuliwaambia wanafunzi wachore picha. Huko Uganda walichora picha za vitu vilivyowafurahisha au kuwachukiza wawapo shuleni. Nchini Tanzania walichora katuni tatu zikionyesha "shughuli nilizokuwa nikifanya kabla ya kuja hapa chuoni; kitu ninachopenda kufanya zaidi hapa chuoni na shughuli nitakazofanya baada ya kumaliza chuo."

## Maigizo

Huko Tanzania wanafunzi walifanya maigizo mafupi kuhusu: mwalimu mzuri, mwalimu mbaya na mwanafunzi mbaya.

## Majadiliano

Nchini Tanzania wanafunzi walikuwa na majadiliano kuhusu wajibu wa walimu, wazazi na wanafunzi katika kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata elimu jumuishi iliyo bora.

## Filamu

Vitendo vyote vilivyofanyika vilipigwa picha. Filamu inayoambatana na kitabu hiki inaonyesha wanafunzi wakifanya mradi wa **Sauti za Vijana** wakiwa madarasani, wakicheza na marafiki zao wakisoma na wakifanyiwa usaili.

## Nani walioshiriki?

Jumla ya wanafunzi 55 walishiriki:

- Shule ya Sekondari Rock, Tororo Uganda – wanafunzi 25, wasichana 15 na wavulana 10.
- Shule ya Msingi Agururu, Tororo Uganda – wanafunzi 16, wasichana 7 na wavulana 9.
- Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa, Morogoro Tanzania – wanafunzi 14, wasichana 8 na wavulana 6.

Katika kila shule kulikuwa na mchanganyiko wa wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu, na mchanganyiko wa wasichana na wavulana. Walijumuishwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo,ulemavu wa akili, wasioona, wenye uoni hafifu na viziwi.

## Shule

Shule zote zinajitahidi kuwa jumuishi. Shule ya Msingi ya Agururu ilifuguliwa mwaka 1980. Katika mwaka 1996 kitengo maalum cha wanafunzi wenye ulemavu kilifunguliwa shuleni hapo. Hata hivyo shule hiyo sasa hivi inaelekeza nguvu zake kuwa jumuishi, ili watoto wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu wasome pamoja. Sasa hivi ina jumla ya wanafunzi 718, kati yao 174 wana ulemavu.

Shule ya Sekondari Rock ni shule yenye fursa sawa kwa wanaomaliza shule za msingi. Katika mwaka 2006 Shirika la Operation Days Work liliwapatia walimu mafunzo ya elimu jumuishi kupitia mradi wa kuendeleza vijana. Tangu hapo walimu na wanafunzi wameshirikiana kuifanya shule kuwa jumuishi kwa wanafunzi wote. Shule hiyo ina idadi ya wanafunzi 180 wenye ulemavu kati ya jumla ya wanafunzi 2,871.

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa kinatoa mafunzo ya ufundi kwa vijana wenye ulemavu na wasio na ulemavu kutoka maeneo ya vijijini. Baadhi ya vijana hao hawakumaliza elimu ya msingi wala sekondari kwa hiyo chuo kinawaendeleza kielimu. Chuo kinahimiza vijana kusaidiana katika masomo au wakati wa mapumziko muda wote wanapokuwa chuoni.



Washiriki kutoka Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa



Washiriki kutoka Shule ya Msingi Agururu



Washiriki kutoka Shule za Sekondari Rock

## Ni mafanikio au matatizo gani yaliyotokana na mradi huu?

Wanafunzi walipiga picha nzuri sana na kuchora michoro mizuri. Pia walijadili mambo mbali mbali yanayohusiana na elimu jumuishi na kutoa maoni na mapendekezo yao.

Baadhi ya wanafunzi walikuwa na aibu sana mradi ulipoanza. Mradi ulifanyika kwa muda wa takribani siku tano katika kila shule. Lakini hata kwa muda huu mfupi baadhi ya wanafunzi waliokuwa na aibu walibadilika na kuweza kutoa maoni yao na wanavyojisikia. Mradi huu ulionyesha walimu kuwa wanafunzi wanaweza kuwa wazuri sana katika kujadili mambo yanayoathiri kujumuishwa kwao katika elimu. Hii pia imewakumbusha watu wazima jinsi ilivyo muhimu kusikiliza maoni ya vijana kuhusu elimu.

Kwa kuwa mradi ulikuwa mfupi sana, hapakuwa na muda wa kutosha kwa kila mwanafunzi aliyeshiriki kujijengea uwezo na kujiamini wakati wa kufanya vitendo hivi vipya na kuongea na wageni wasiowafahamu. Kwa hiyo baadhi yao huenda hawakuweza kutueleza mengi kama ambavyo wangependa



**Mfano wa Bango lililowekwa picha kutoka Shule ya Msingi Agururu.**

Lugha ilikuwa pia tatizo, hususan katika shule ya msingi ya Agururu. Katika shule hii, wanafunzi wanaongea lugha saba za asili tofauti na hawakuwepo wakalimani wa lugha zote wakati wa mradi. Masomo yote shuleni yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza kwa hiyo wanafunzi walifanya mradi kwa kiingereza. Lakini iliwawia vigumu kupata maneno sahihi, hasa walipojaribu kuongea juu ya maoni mapya au wanavyojisikia kuhusiana na kujumuishwa au kutengwa.

## Tulipangaje mambo waliyosema wanafunzi?

Wanafunzi walioshiriki katika mradi wa Sauti za Vijana walipiga picha takribani 200 na kuchora michoro mingi. Waliongea na kuandika mengi kuhusu maoni yao katika kujumuishwa au kutengwa kwenye elimu. Kwa bahati mbaya hatuwezi kuchapisha kila kitu hapa.

Kwa hiyo tulichagua picha na michoro ambayo wanafunzi waliweza kuieleza kwa usahihi. Pia tulichagua picha zitakazoonekana vizuri katika kitabu.

Picha na misemo vimepangwa katika sehemu tano – mazingira, sera, matendo, rasilimali na mitazamo. Haya ni maeneo muhimu ambayo wanafunzi wameona yanahitaji mabadiliko ili elimu iwe jumuishi zaidi kwa kila mmoja.

# Maoni ya wanafunzi kuhusu elimu jumuishi

## Mazingira

Mazingira ya ndani na yale yanayozunguka shule yanaweza kuathiri wanafunzi kuwepo au kutokuwepo kwao shuleni. Picha walizopiga wanafunzi zinaonyesha mambo mengi kuhusu mazingira ambayo ni muhimu kwao.

Mambo hayo ni pamoja na; hali ya madarasa, kuwepo kwa mahali pa ukimya pa kusomea au kukutana na marafiki, kama wanaweza kuzunguka shuleni kwa urahisi na kama kuna vyoo vinavyoingilika na visafi.

Kinachoonyeshwa kwa uwazi kwenye picha walizopiga wanafunzi ni kwamba kila mmoja ana mahitaji yake na maoni kuhusu kinachofanya mazingira kuwa rafiki na kufikika.



**“Napenda eneo hili. Pana ubaridi hapa. Hapa ndipo tunapokutana na marafiki zetu wakati wa maongezi. Ni mahali pazuri pa kutuliza mawazo na kupumzika.”**

Ally Iddi, mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

Picha na Ally Iddi



**“Kuna mawe makubwa hapa ardhini. Tunaweza kuyaangukia.”**

Issac Otedo, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Msingi Agururu

**“Haya mawe makubwa hayatakiwi kuwa hapa. Watoto wanaweza kutupiana wakati wanapopigana.”**

Michael Hashaya , mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Msingi Agururu.


Picha na Isaac Otedo



"Sipendi msitu huu. Ni mnene na miti imesongamana. Pia uko karibu sana na bweni la wavulana kwa hiyo unaleta wadudu wabaya na nyoka pia."

Aron Nducha, mwanafunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

Picha na Aron Nducha



"Napenda kuangalia mwamba ule. Kauli mbiu ya shule yetu inasema 'kwea mpaka kileleni'. Mwamba unawakilisha shule yetu na kuonyesha uzuri wake. Mwamba huu umeipa shule jina lake na kutuhamasisha tufanye bidii tufike kileleni katika masomo yetu."

Florence Asabit, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock.

Picha na Florence Asabit



"Kuna msongamano madarasani. Shule inapokea wanafunzi wengi...(Hapa) watu wanafanya kazi... wanaboresha hadhi ya shule. Wanajenga madarasa mapya. Jengo hilo litakuwa na mabwalo na maktaba nyingine."

Wiliam Osinde, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock

Picha na William Osinde



"Jengo hili jipya linaonekana ni zuri. Ndilo jengo zuri kuliko yote hapa shuleni. Ninajisikia vizuri ninapokuwa kwenye jengo hili. Lakini nafurahi kwa sababu darasa langu liko chini. Nisingeweza kupanda ngazi endapo darasa langu lingekuwa ghorofani."

Irene Athieno, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Sekondari Rock.

Picha na Irene Athieno




**“Bweni hili ni safi. Usafi unazuia magonjwa.”**

Isaac Otedo, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Msingi Agururu.

**“Bweni hili ni zuri kwa sababu lina kitanda kizuri ninacholalia. Na sanduku linahifadhi vitu vyangu kwa usalama.”**

Lukuman Mutoto, mwanafunzi kiziwi, Shule ya Msingi Agururu.

Picha na Issac Otedo



**“Napenda picha hii ya darasa kwa sababu inaonyesha mazingira mazuri na ni hapo tunajifunza mambo mbali mbali.”**

Mwajuma Tepe Tepe, mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

Picha na Mwajuma Tepe Tepe




Picha na Winny Auma



Picha na Scovia Awino

**“Hiki choo ni kibaya. Ni vigumu mimi kukitumia bila kugusa uchafu.”**

Scovia Awino, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo

**“Wanatakiwa kujenga choo kingine kwa sababu hiki kinakaribia kujaa. Au kama hawawezi kujenga kingine itabidi wasafishe hiki.”**

Victoria Esaete, mwanafunzi.

**“Kwa mara nyingi hasa kwenye hosteli inaniwia vigumu kwa kuwa hakuna choo kinachonifaa mimi mwenye ulemavu wa viungo.”**

Moses Ochom, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Sekondari Rock

## Sera

Kanuni zinazotawala shule au mfumo wa elimu vinaweza kuathiri mitazamo ya watu au tabia. Hii inaweza aidha kusaidia au kuzuia wanafunzi kujumuishwa.

Hatukuwaambia wanafunzi wajadili sera za elimu, lakini maoni yao yametupa ushauri kuhusu ni nini kinachopelekea sera ya elimu jumuishi kuwa nzuri au mbaya.

Walitaja mambo mengi ambayo watunga sera wanatakiwa kuyazingatia, kuanzia dini, lugha hadi ulemavu na utayarishaji wa vipindi.

**"Katika shule hii kila dini inatambulika na tunaruhusiwa kuabudu bila bughudha.Hili linanifanya nijisikie kujumuishwa."**

Emmanuel Papaok, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Sekondari Rock.

**"Wote tunalipa ada sawa bila kujali lugha anayoongea ye yote au nchi anayotoka. Katika shule hii kila mmoja anakaribishwa bila kujali uraia wake."**

John Ojiro, Shule ya Sekondari Rock.

**"Najisikia kujumuishwa katika shule hii kwa sababu nina uhuru wa kujieleza,kuongea na kujongea."**

Juliana Atwine, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock.

**“Najisikia kutojumuishwa kwa sababu sipendi kukaa hapa shuleni kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa moja jioni. Inanifanya nichukie shule hii kwa sababu sipewi muda wa kupumzika.”**

Alex Awori, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock.

**“Kuna masomo mengi sana hapa na hii inanifanya nijisikie kutojumuishwa.”**

Hellen Nalubanga, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock.

**“Katika darasa hili najifunza na marafiki zangu tukiwa tumechanganyika. Siyo kutenganishwa kwamba wenye ulemavu kaeni kule na wasio na ulemavu wakat hapa. Hapana, tunachanganyika na hii inanifanya nifurahi.”**

Isaac Otedo, mwanfunzi mwenze ulemavu wa viungo. Shule ya Msingi Agururu.

## Matendo

Jinsi mambo yanavyofanyika shuleni yanaweza kuashiria kama wanafunzi wanashirikishwa katika hatua za kujifunza au la. Wanafunzi walioshiriki katika mradi wa **Sauti za Vijana** walitueleza kuhusu njia mbali mbali za kufundishia au kujifunzia ambazo zinaweza kuwasaidia katika kupata elimu bora zaidi.

Walitaja umuhimu wa kuwahamasisha wanafunzi kusaidiana wenyewe kwa wenyewe katika masomo na shughuli za burudani na siyo kila wakati kutegemea walimu au watu wengine wazima.

Wanafunzi walielezea pia maoni yao kuhusu kuwa wachangamfu na kujumuika katika masomo, na sio kusikiliza tu na kukaa kimya wakati mwalimu anapofundisha.

Pia waliweka msisitizo kuhusu kuwepo kwa muda wa kupumzika na kuwa na marafiki. Hii itasaidia sana kujiona wanajumuishwa na itaboresha mafanikio yao katika elimu wanayopata.




Mchoro na Wiliam Osinde Shule ya Sekondari Rock

**“Tunatakiwa tushirikiane na kuomba msaada kwa wanafunzi wenzetu. Tusisubiri tu mwalimu – marafiki zetu wanaweza kutuelezea pia”.**


Mwajuma Tepe Tepe, mwanafunzi mwenye Ulemavu wa akili Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

**“Tunatakiwa kuulizana maswali sisi wenyewe kwa wenyewe. Darasani kama hakuna mwalimu tunatakiwa kusaidiana sisi wenyewe”.**

Witness Ngimbuch, mwanfunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

**“Kuna wanafunzi wengi hapa shuleni. Tunaweza kuunda vikundi vya majadiliano na kujadiliana kazi zetu”.**

James Okello, mwanafunzi Shule ya Sekondari Rock.



**“Napenda maktaba hii, imepangwa vizuri. Mwalimu anapofundisha unaweza kusahau, lakini kama ukijisomea mwenyewe unaweza kukumbuka mambo mengi zaidi.”**

Dickson Msemo, mwanafunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

**“Tunakwenda maktaba kusoma. Tunaangalia runinga, tunajifunza vitu mabali mbali na baadae tunakuwa na midahalo na majadiliano kuhusu mambo tuliyosoma au kuona.”**

Mwajuma Ally, mwanafunzi mwenye ulemvu wa uoni. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

Picha na Dickson Msemo



**“Hii ni karakana ambako tunajifunza shughuli za useremala.”**

David Mgowano, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

**“Hapa tunajifunza utaalamu wa aina mbali mbali, jambo ambalo ni zuri kwa maisha yetu ya baadae.”**

Euphrosina Nkinga, mwanafunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

Picha na David Mgowano



"Maabara ya sayansi ni mahali tunapofanya majaribio kwa vitendo. Mambo mengi ni ya nadharia, lakini tunapopata nafasi ya kufanya majaribio inatusaidia kujifunza jinsi ya kutengeneza vitu tunavyotumia katika jamii kwa wakati huu."

Alex Awori, mwanafunzi,
Shule ya Sekondari Rock.

Picha na Alex Owori



"Tunapata habari katika runinga iliyoko katika maktaba. Wakati ninapoitazama napata habari za mambo mbali mbali yanayoendelea duniani."

Omari Chota, mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

Picha na Omari Chota



"Tunatumia eneo hili mara chache tukiwa na vikundi vya majadiliano au midahalo. Kwa mfano, tunaweza kuwa na mjadala, 'Je kupata fedha kuna manufaa kuliko kupata elimu?' Wale wanaosema ni bora kupata elimu wanashinda mjadala huu hadi sasa hivi."

Tausi Saidi, mwanafunzi Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa.

Picha na Tausi Saidi



"Huu ni mlango wa chumba alichokuwa akiishi mwanafunzi mwenzetu aliyefariki dunia. Ninamkumbuka kila ninapouona mlango huu."

Mariam Abadallah, mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

Picha na Mariam Abdallah

**“Kushiriki katika vitendo kama kuimba na dansi kunanifanya nijisikie ninajumuishwa.”**

Scovia Awino, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Sekondari Rock.

**“Marafiki wengi wananifanya nijisikie ninajumuishwa hapa shuleni kwa sababu wananisaidia ninapokuwa na kazi ngumu.”**

Rachael Nadunga, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock.



Wanafunzi wakicheza mchezo wa kriketi, Shule ya Msingi Agururu. Picha na Claire Nagami




Mchoro na Lukuman Mutoto, mwanafunzi kiziwi, Shule za Msingi, Agururu

# Rasilimali

Upatikanaji wa rasilimali unaweza kwa kiasi kikubwa kuathiri kuwepo kwa wanafunzi, kushiriki kwao na kufanikiwa katika kupata elimu.

Wanafunzi walioshiriki katika mradi wa **Sauti za Vijana** walitoa angalizo kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa chakula na maji kwa ajili yao kama watajumuishwa katika kupata elimu.

Waliongea kuhusu jambo hili zaidi kuliko walivyoongea kuhusu kuwepo kwa rasilimali, kama vitabu, madawati au majengo yenye mitelemko inayopitika kwa kila mtu.



"Bomba hii inaturahishia kupata maji na mtaro wa kupitisha maji ni mzuri. Hali hii ni nzuri kwa sababu tunaweza kupata maji kwa utulivu. Ni vizuri kuwa na mtaro kwa sababu maji yanayopita hutumika kunyweshea shamba la migomba."

Lukuman Mutoto, mwanafunzi kiziwi, Shule ya Msingi Agururu.

Picha na Lukuman Mutoto



"Hili tangi ni zuri kwa kuwa linatusaidia kuvuna maji ya mvua. Kama hakuna mvua bado tunakuwa na maji safi ya kunywa. Wakati mwingine kama hakuna maji ya kutosha kwenye tangi tunakwenda kijijini kuchota maji. Ni kazi ngumu."

Winny Aumna, mwanafunzi kiziwi, Shule ya Msingi Agururu.

Picha na Winny Auma



Mchoro na Pauline Awori

**“Najisikia kujumuishwa kama nikikosa chakula (kwa sababu hakuna chakula cha kumtosha kila mmoja) ninakwenda kwa mmoja wa walimu wangu nae mwamamume/ mwanamke hunipa pesa nami nakwenda kununua chakula changu. Kwa hiyo najisikia napendwa hapa shuleni. Najisikia kutojumuishwa ninapokosa chakula cha mchana na mwalimu anayehusika akaniambia kwamba ‘hakuna tatizo, wewe ni mnene kwa hiyo huna haja ya kula’. ”**

Pauline Awori, mwanafunzi, Shule ya Sekondari, Rock.

**“Wakati mwingine kuna chakula kisichokuwa na lishe hapa shuleni kuliko nyumbani. Kuna shida ya kupata chakula na maji kwa kuwa mstari wa foleni ni mrefu.”**

Mary Amoding, mwanafunzi Shule ya Sekondari, Rock.




Picha na Ismail Etyang



"Nilipiga picha hii kwa sababu inaonyesha mazingira yasiyokuwa masafi. Inaonyesha kwamba chakula kinachopikwa hapa hakina afya na kinaweza kuleta magonjwa mbali mbali pamoja na kuharisha. Mwanafunzi anaweza kuathirika kimasomo kama anaharisha atakuwa akitoka darasani mara kwa mara na kukosa somo. Hii itamfanya mwanafunzi kushindwa darasani na kupewa adhabu atakapokutwa nje ya darasa."

Juliana Atwine, mwanafunzi,
Shule ya Sekondari, Rock.

Picha na Juliana Atwine

“Kinachonifanya nijisikie kutojumuishwa katika shule hii ni kwa sababu wazazi wangu ni maskini, hawawezi kuninunulia vitabu vya kutosha. Jambo hili linafanya maisha yangu kuwa magumu hapa shuleni.

Hawawezi pia kuninunulia kila kitu ninachohitaji hapa shuleni kama nguo. Kuwa shuleni bila vitabu na kalamu kunanifanya nijisikie kutojumuishwa kwa sababu walimu walikuwa wakinitoa nje ya darasa kwa kuwa sikuwa na vitabu vya kuandikia.”

Jackline Auma. mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock.

“Mimi ninakosa raha ninapoona wanafunzi ambao ni maskini.”

Blantina Nyachwo, mwanafunzi kiziwi, Shule ya Msingi Aguruzu




Mchoro na Blantina Nyachwo

# Mitazamo

Mitazamo ya watu wengine inaweza aidha kuwatia moyo au kuwakatisha tamaa wanafunzi kuhudhuria shuleni.

Wanafunzi walioshiriki katika Mradi wa **Sauti za Vijana** walieleza kwamba wanataka wazazi wao wawatie moyo na kuwasaidia ili wapate elimu.

Walieleza kwamba mitazamo yao na ya wanafunzi wenzao, inaweza kuathiri kushiriki kwao na kupata mafanikio katika elimu.

Mitazamo ya walimu, wakuu wa shule na wafanya kazi wengine pia ilitajwa na wanafunzi kuwa ni muhimu sana katika kuwasaidia kuingia shuleni na kunufaika na elimu wanayopata kwa uwezo wao wote.

John Ojiro kutoka Shule ya Sekondari Rock amechora picha iliyoko (kulia) kuhusu mitazamo ya wanafunzi inavyoweza kuwafanya wengine wakajisikia kutokaribishwa shuleni:

Kukosa furaha baada ya kutengwa pamoja na unyanyapaa.

“Mungu kwa nini?!! Nifanye nini? Hata rafiki zangu wananikataa!!”

“Mwangalie yule mjinga wa kidato cha kwanza. Anawezaje kuniita mimi! Nina muda wa kuambatana nae?”



**Kama mzazi ana mtoto mwenye ulemavu, anatakiwa ampeleke shule, kwa sababu wazazi wengine huwaacha watoto wao nyumbani. Lakini wawapeleke shuleni.”**

Tausi Saidi, mwanafunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

**“Wazazi wanatakiwa walete barua ya kusema “mwanangu angependa kujifunza mafunzo ya ufundi.”**

Omari Chota, mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

“Kama mtu mwenye ulemavu, pia nahitaji kuwa na maisha mazuri hapo baadae ili niweze kutunza familia yangu. Katika dunia yetu hii inahitajika angalau mtu awe amekwenda shule na aonekane kama binadamu. Na nahitaji kujifunza jinsi ya kushirikiana na watu wengine katika nyanja mbalimbali, ili kuondokana na hatari ya kutokushirikiana na watu wengine katika jamii, shule na jumuia kwa ujumla”.

Moses Ochom, mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo, Shule ya Sekondari Rock.

“Tufanye kazi kwa bidii kama wanafunzi. Tujitahidi ili kupate elimu tuliyofuata hapa.”

Teresia Kisawani, mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

“Tuna watu wenye mahitaji maalum hapa. Kama tukimwona mtu mwenye matatizo tuwe wavumilivu na kumsaidia – hatufanani wote.”

Dickson Msemo, mwanafunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

**"Mwalimu anatakiwa awapende wanafunzi wake".**

Ally Iddi, mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

**"Ninasikilizwa, hasa wakati wa kuuliza maswali ambayo sijui (majibu yake). Wao (walimu) huyajibu bila kubabaisha".**

Alex Awori, mwanafunzi, Shule ya Sekondari, Rock.

**"Katika shule yangu ya nyuma walimu na wanafunzi walikuwa wakinicheka niliposhindwa kusema kitu, kwa kuwa sikuweza kutamka maneno nao hawakuniruhusu kuongea. Lakini katika shule hii, kama wanafunzi wakinicheka walimu huwakemea nao huniomba msamaha".**

Pauline Awori, mwanafunzi, Shule ya Sekondari Rock

**"Mwalimu mzuri ni yule anayetambua kuwa kuna wanafunzi wenye mahitaji maalum na yuko tayari kuwasaidia".**

Dickson Msemo, mwanafunzi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa



**"Hii ni ofisi ya Mkuu wa Chuo, ninaipenda. Kila ninapokuwa na tatizo naingia humu nae ananisaidia".**

Nassoro Kasebeya, mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili, Cho cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

Picha na Nassoro Kasebeya

# Baadhi ya mawazo ya mwisho...

**"Tunahitaji kupendana"**
Aron Nducha, mwanafunzi, Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa

**"Kuwa katika shule jumuishi kunatuwezesha kujifunza kusaidiana na pia kuelewa kuwa elimu ni kwa kila mmoja..."**

Pauline Awori, mwanafunzi, Shule ya Sekondari, Rock.

**"Kwangu mimi kujumuishwa ni kuwa sehemu ya kitu fulani...kama kuwa sehemu katika shughuli mbalimbali na katika jamii kama kucheza mpira wa miguu/kandanda kupata elimu, muziki, dansi na maigizo."**

Juliana Atwine, mwanafunzi, Shule ya Sekondari, Rock.Rock High School

**"Tunahitaji kusikiliza kama tunataka kuelewa..."**
Angel Kejo, mwanafunzi, Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi, Bigwa.

# Sauti za Vijana

## Maoni ya Vijana kuhusu Elimu Jumuishi

"Kitabu hiki chenye picha, michoro na maoni ya vijana kinaonyesha juhudi za kufanya elimu jumuishi kupatikana kwa uhakika. Mambo yaliyozungumzwa na vijana yanajumuisha sera, mitazamo, tabia hadi ugawaji wa rasilimali na mazingira.

Kitabu hiki kimenipa hamasa na changamoto ya kuwajibika pamoja kwa vitendo na watunga sera wa elimu, mameneja, viongozi, walimu, wazazi, wahudumu na wanafunzi katika kubadili mitizamo ya mahitaji ya kielimu kwa watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu.

Moses Moiza, Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii - Idara ya Ulemavu na Wazee, Tororo, Uganda.

**The Atlas Alliance**
Schweigaardsgt 12
PO Box 9218 Grønland
0134 Oslo, Norway
Tel: +47 22 17 46 47
Fax: +47 23 16 35 95
Email: atlas@atlas-alliansen.no
Website: www.atlas-alliansen.no

the atlas alliance
global support to disabled people